

**JEDWALI LA MAREKEBISHO YA RANDAMA YA MAELEWANO (MoU) YA  
WADAU WA TASNIA YA KAHAWA YA MWAKA, 2011**

<b>Na</b>	<b>KIFUNGU</b>	<b>MAREKEBISHO YANAYOPENDEKEZWA</b>	<b>SABABU</b>
1	<b>Kifungu cha 2.0</b>	<p>Randama inafanyiwa marekebisho katika Kifungu cha <b>2.0</b> kwa</p> <p>(a) Kukiboresha kifungu cha <b>2.2</b> na kusomeka kama ifuatavyo:-</p> <p><b>2.1.</b> Wadau wamekubaliana pia kwamba utaratibu utakaotumika kugharamia maendeleo ya zao la kahawa ni kwa kuanzisha na kutumia Mfuko wa Wakfu (Trust Fund). ”</p> <p>(b) Kukiboresha kifungu cha <b>2.3</b> na kusomeka kama ifuatavyo:-</p> <p><b>2.3.</b> Mfuko wa wakfu utakaoanzishwa utatumika kugharamia majukumu ya pamoja ya kuendeleza zao la kahawa ikiwemo huduma za ugani, utafiti, uendelezaji masoko, uzalishaji wa miche bora, upatikanaji wa pembejeo na huduma zingine kwa kiwango na utaratibu utakaokubalika na wadau.”</p>	Kuifanya randama kuwa na tafsiri inayokusudiwa.
2.	<b>Kifungu cha 4.0</b>	<p>Randama inafanyiwa marekebisho katika Kifungu cha <b>4.0</b> kwa Kukiboresha na kusomeka kama ifuatavyo:-</p> <p><b>4.1.</b> Wadau wanakubaliana kwamba fedha za mfuko zitatumika kwa ajili ya kugharamia majukumu ya pamoja kwa kiwango na utaratibu ufuatao:-</p> <p><b>4.1.1.</b> Fedha zitakazochangwa na wadau kwa ajili ya kugharamia majukumu ya pamoja zitagawanywa na kutumika kwa viwango vifuatavyo:-</p> <p>(i) Asilimia 1 (1%) ya fedha zinazotokana na mauzo ya kahawa zitatumika kwa ajili ya kugharamia shughuli za utafiti na upatikanaji wa miche bora ya kahawa;</p>	Kuifanya randama kuwa na tafsiri inayokusudiwa.

		<p>(ii) Asilimia 0.2 (0.2%) ya fedha zinazotokana na mauzo ya kahawa zitatumika kwa ajili ya shughuli za mnada na kuiwezesha Bodi kusimamia utekelezaji wa majukumu ya pamoja; na</p> <p>(iii) Asilimia 1 (1%) ya fedha zinazotokana na mauzo ya kahawa zitaumika kwa ajili ya kugharamia kazi za Mfuko wa wakfu.</p> <p><b>4.1.2</b> Wadau wanakubaliana pia kwamba mtu au taasisi yoyote itakayopewa fedha kwa ajili ya kugharamia majukumu ya pamoja itapaswa kuzingatia taratibu zitakazoanishwa na Mfuko wa Wakfu.</p> <p><b>4.1.3</b> Bila kuathiri Kipengele cha <b>4.1.1</b> cha Randama hii, fedha za Mfuko wa Wakfu zinaweza kutumika kugharamia majukumu mengine ya pamoja iwapo wadau wataazimia kupitia mkutano wa wadau.</p>	
3.	<b>Kifungu cha 5.0</b>	<p>Randama inafanyiwa marekebisho katika Kifungu cha <b>5.0</b> kwa Kukiboresha na kusomeka kama ifuatavyo:-</p> <p><b>5.1.</b> Wadau wanakubaliana kwamba Mfuko wa Wakfu utasimamiwa na Bodi ya Wadhamini ambayo itakakuwa na wajumbe saba (7) watakaowakilisha wadau kama ifuatavyo:-</p> <p>(i) Wajumbe watatu (3) watakaochaguliwa na wadau kuwakilisha wakulima kutoka Nyanda za Juu Kusini, Kanda ya Ziwa na Kanda ya Kaskazini;</p> <p>(ii) Wajumbe wawili (2) watakaoteuliwa kuwakilisha Chama cha Wafanyabiashara wa Kahawa (TCA);</p> <p>(iii) Mjumbe mmoja (1) atakayeteuliwa na Wizara kuwakilisha Serikali; na</p>	Kuifanya randama kuwa na tafsiri inayokusudiwa.

		<p>(iv) Mjumbe mmoja (1) atakayeteuliwa miongoni mwa Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri za Wilaya zinazolima kahawa kwa nafasi yake.</p> <p><b>5.2</b> Wajumbe wa Bodi ya Wadhamini watakaa kwa kipindi cha miaka mitatu (3) na wanaweza kuchaguliwa au kuteuliwa tena kuwa wajumbe.</p>	
4.	<b>Kifungu cha 6.0</b>	<p>Randama inafanyiwa marekebisho katika Kifungu cha <b>6.0</b> kwa Kukiboresha na kusomeka kama ifuatavyo:-</p> <p>(a) Kufuta vifungu vya <b>6.1, 6.2, na 6.4</b> vya Randama:-</p> <p>(b) Kukiboresha kifungu cha <b>6.3</b> na kusomeka kama ifuatavyo:-</p> <p><b>6.1</b> Randama hii itadumu kwa kipindi cha miaka mitatu (3) kuanzia tarehe ya kusainiwa na inaweza kufanyiwa marekebisho na wadau kupitia Mkutano Mkuu wa wadau.</p> <p><b>6.2</b> Marekebisho yatakuwa na nguvu ya kisheria iwapo marekebisho hayo yataidhinishwa na wadau na kufanywa kwa maandishi na kusainiwa na wahusika wa Randama.</p>	Kuifanya randama kuwa na tafsiri inayokusudiwa.
5.	<b>Kifungu cha 8.0</b>	<p>Randama inafanyiwa marekebisho katika Kifungu cha <b>8.0</b> kwa Kukiboresha anuani za wadau kuwa anuani za wahusika wa Randama</p>	Kuifanya randama kuwa na tafsiri inayokusudiwa.